# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA KUMI NA SABA

**05 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA KUMI NA SABA – TAREHE 05 MEI, 2025

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### WAZIRI WA UJENZI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**210. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, kwa nini Wastaafu hawapewi haki zao mara tu wanapostaafu.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**211. MHESHIMIWA BALOZI LIBERATA RUTAGERUKA MULAMULA (KUTEULIWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kukarabati Shule Kongwe za Msingi na Sekondari - Misenyi.

**212. MHESHIMIWA JOSEPH ANANIA TADAYO (MWANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali kupitia TARURA ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Mangio hadi Kivizini Wilayani Mwanga.

**213. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali italipa madeni ya Walimu wa Shule za Sekondari waliohamishiwa Shule za Msingi.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**214. MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS NDAKIDEMI (MOSHI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, upi mpango wa Taifa wa kupanda miti kwa kipindi cha muda mfupi na mrefu ili kukabiliana na janga la kukata miti.

**WIZARA YA NISHATI:**

**215. MHESHIMIWA SAADA MANSOUR HUSSEIN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha matumizi ya mkaa mbadala yanaenezwa hadi Zanzibar.

**WIZARA YA FEDHA:**

**216. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, kuna mpango gani wa kusitisha kutoa vibali kwa mashine za Kamari ili kupunguza umaskini kwa Vijana.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**217. MHESHIMIWA VINCENT PAUL MBOGO (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Vituo vya Polisi Kata za Kate na Kipande kwani tayari maeneo yameandaliwa.

**218. MHESHIMIWA ZAHOR MOHAMMED HAJI (MWERA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali imejiandaaje kukabiliana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu na Madawa ya Kulevya kwani mbinu za uhalifu zimebadilika.

**WIZARA YA MADINI:**

**219. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Halmashauri ya Mpanda inanufaika vipi na mauzo ya mchanga wa marudio ya madini katika Kata ya Misunkomilo – Mpanda.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**220. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti maudhui yasiyo na maadili katika mitandao ya kijamii kwa maslahi ya afya ya akili na Watoto.

**221. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali inafanya maandalizi gani kuhakikisha nchi yetu inafanya vizuri katika Mashindano ya AFCON 2027.

**WIZARA YA KILIMO:**

**222. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia Redio za Kijamii kutoa elimu ya matumizi bora ya Viuatilifu katika Zao la Korosho.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**223. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani kuwasadia Wananchi wa Kata za Ngarambe na Mwaseni - Rufiji kukabiliana na Wanyama waharibifu hasa Tembo.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**224. MHESHIMIWA DKT. MEDARD MATOGOLO KALEMANI (CHATO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Ujenzi wa Tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam cha masuala ya Samaki eneo la Kasagara - Chato ulioanza 2021 utakamilika.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA UJENZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**DODOMA**<br>**05 MEI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**<br>**KATIBU WA BUNGE**